


- Una ugonjwa kali ya ghafula
- Unaganda uso, miguu, au mikono
- Umechomeka sana
- Umeumia kichwa
- Una mtoto aliyejeruhiwa

Usiende kwa ER kwa sababu ya:

- Kuumwa na sikio
- Homa, kukohoa, au mafua
- Kuchomeka (kidogo)
- Kutenguka
- Chanjo
- Sindano za mafua
- Kuumwa na koo

Katika hali ya dharura piga 911:



**Huduma ya Matibabu
nchini Amerika
(Medical Care in the
United States)**

(Swahili)



www.refugees.org

*Protecting Refugees, Serving Immigrants,
Upholding Freedom since 1911*

HABARI YA MAWASILIANO:

riht@uscridc.org

**U.S. Committee for Refugees and
Immigrants**

1717 Massachusetts Ave., NW
Suite 200

Washington, DC 20036

Simu: 202 • 347 • 3507

Faksi: 202 • 347 • 7177

www.refugees.org

*Brosha hii ilitengenezwa na ufadhili kutoka kwa
Idara ya Afya na Ofisi ya Huduma za Wanadamu
ya Kuwapatia Wakimbizi makazi mapya.*

HUDUMA YA MATIBABU NCHINI AMERIKA

Nchini Amerika kuna njia nyingi za kupokea huduma ya matibabu, lakini zinazotumiwa sana ni:

- Kutembelea ofisi ya daktari
- Huduma ya dharura (wakati mwingine inaitwa kliniki za kuingia bila miadi)
- Vyumba vya Dharura (ER)

JE! NI LINI NINAWEZA KUTEMBELEA OFISI?

Kutembelea ofisi ni wakati unafanya miadi ya kuona daktari wako mkuu katika ofisi ya daktari. Panga kutembelea ofisi wakati wa:

- Homa, kukohoa, au mafua
- Kuumwa na sikio
- Sindano za mzio
- Chanjo
- Kuangaliwa mwili kila mwaka

JE! NI WAKATI UPI NINAPASWA KUTUMIA HUDUMA YA DHARURA?

Kliniki za huduma ya dharura au kliniki za kuingia bila miadi ni kama ofisi za madaktari, lakini hakuna miadi inayohitajikana. Badala ya daktari wako mkuu, utamwona daktari yeyote ambaye ako kwenye zamu kwa kliniki ya huduma ya dharura. Kliniki za huduma ya dharura mara kwa mara zinapatikana karibu na hospitali au maduka makubwa, na kwa kawaida huwa zimefunguliwa kwanzia mapema sana asubuhi hadi jioni sana. Unastahili kutumia huduma ya dharura kwa magonjwa au majeraha madogo kama vile:


- Kuumwa na sikio
- Kuchomwa na jua au kuchomwa kidogo
- Homa, kukohoa, au mafua

- Homa ndogo
- Kuangalia mwili shuleni au kazini
- Sindano za mzio

JE! NI WAKATI UPI NINAPASWA KUTUMIA ER?

Vyumba vya Dharura, au ER, viko hospitalini. Mara kwa mara huwa vimefunguliwa masaa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki. ER huwa ghali zaidi ya kutembelea ofisi na huduma ya dharura. Unaweza kusubiri kwa muda mrefu ukienda kwa ER na hali yako si kali. Unapaswa kutumia ER kwa dharura au magonjwa kali tu, kama vile:

- Uchungu wa kifua, kuganda uso, mkono au mguu, au shida ya kuzungumza



- Homa kali na shingo ngumu, kuchanganyikiwa kiakili, au shida ya kupumua
- Upungufu mkali wa hewa (kupata hewa)
- Sumu
- Kupoteza ufahamu kwa ghafula
- Kukohoa au kutapika damu
- Dalili kali, za ghafula au zisizo za kawaida.

UKITUMIA ER:

- 1) Chukua jina la daktari na namba ya simu kwa ER.
- 2) Mwambie muuguzi wa ER na daktari aina ya madawa (tembe) unazotumia.
- 3) Mwamwie muuguzi wa ER au daktari ikiwa una hali ya kimatibabu.

Nenda kwa ER ikiwa:

- Umepoteza ufahamu
- Umevunjika mfupa
- Unakohoa au kutapika damu